BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 19 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Afya:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2026/2027.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

185. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Katika siku za hivi za karibuni, kumejitokeza wimbi kubwa la matukio ya vijana katika jamii yetu ndani ya Zanzibar, kuwadhuru wazazi wao wa kuwazaa kwa kutumia silaha kali. Hali hii inasababishwa na matumizi mabaya na makubwa ya mihadarati mfano bangi, ulevi na uraibu mwengine.

(a) Je, Serikali imechukua jitihada gani kuzuia uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya kwa vijana wa Zanzibar.

(b) Ni lini Serikali itajenga kituo cha kuwasaidia vijana walioathirika na uraibu wa kutumia madawa ya kulevya kwa Unguja na Pemba.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

99. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba ilikuja na mradi mzuri wa Mji Salama, ambapo maeneo mengi ya mji yalifungwa Kamera za Ulinzi (CCTV) ili kuimarisha hali ya usalama ya mji wetu. Hata hivyo, hivi sasa kamera nyingi zimeondolewa kutokana na miradi ya ujenzi wa barabara na zilizobakia hazifanyi kazi.

(a) Je, uendelezaji wa mradi wa Mji Salama umeishia wapi na kwa nini mradi huo umesita kufanyakazi.

(b) Kwa kuwa gharama kubwa imetumika kuweka Kamera za Ulinzi pamoja na miundombinu yake, kwa nini Serikali haioni kuwa kutokufanyakazi kwa mradi huo, kumezipoteza bure fedha za umma.

(c) Je, kuna mpango wowote wa kurejesha tena mradi wa Mji Salama kwa kuwa bado matukio mengi ya kiuslama yanatokea katika mji na mitaa yetu.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

111. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Katika eneo la Darajani mkabala na Maegesho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), kumewekwa maduka na Kituo cha Mabasi ambapo ndani yake kuna kiwanja cha michezo cha watoto. Hata hivyo, kiwanja hicho mpaka hivi sasa bado hakijafunguliwa na watoto wa maeneo ya Mchangani, Mbuyuni, Malindi na maeneo ya jirani, wanahangaika kupata eneo la kucheza.

Je, ni lini kiwanja hicho kitafunguliwa ili watoto waweze kupata haki yao ya kucheza na kuwaepushia usumbufu.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

146. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kumejitokeza malalamiko ya wananchi kupoteza ardhi zao kwa ajili ya uwekezaji bila ya kulipwa fidia ya haki au kuchelewa kulipwa.

Je, Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha fidia za haki za wananchi zinalindwa katika mchakato wa uwekezaji.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

18. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Takribani miaka miwili sasa tokea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipoingia katika makubaliano na Kampuni ya *Africa Global Logistic* (AGL) kuiendesha Bandari ya Malindi ili kuongeza ufanisi zaidi wa utoaji wa huduma bandarini hapo.

(a) Je, ni vifaa vipi vilivyokuwepo kabla ya bandari hiyo kupewa Kampuni ya AGL.

(b) Je, ni vifaa vipi vilivyoongezeka baada ya bandari hiyo kupewa Kampuni ya AGL kwa lengo la kuimarisha huduma.

(c) Je, hali ya uingiaji na utokaji wa mizigo bandarini hapo umeongezeka kwa kiasi gani baada ya bandari hiyo kupewa Kampuni ya AGL.

134. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Natambua jitihada mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza miradi ya maendeleo ikijumuisha miradi ya ujenzi.

(a) Je, Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha miradi hiyo inakuwa rafiki na wezeshi kwa Watu Wenye Ulemavu kwa kuondoa vikwazo katika matumizi ya miradi hiyo.

(b) Je, Wizara inachukua hatua gani kwa miradi ambayo inatekelezwa bila ya kuzingatia mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu hususani wakati wa ujenzi wake.

(c) Wizara yako inachukuwa hatua gani kuhakikisha miradi hiyo inatumika bila ya usumbufu kwa Watu Wenye Ulemavu baada ya kumalizika kwake.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

80. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wananchi wa Magomeni wanaishukuru Serikali kupitia Kampuni ya Usambazaji Maji ya *RAND WATER* kwa ushirikiano waliopatiwa katika kutengeneza njia mbadala za kusambaza maji kutokana na uharibifu wa bomba kuu katika harakati za ujenzi wa miradi ya 'flyover' ya Thabit Kombo (Mwanakwerekwe), bomba lililokuwa linasambaza maji katika shehia ya Kwamtumwajeni, Nyerere, Sogea, Magomeni na Meya.

(a) Pamoja na kuwa mradi wa *'flyover'* wa Thabit Kombo upo katika hatua nzuri ya maendeleo, je, ni lini mabomba mapya yatamalizwa kulazwa na kuanza kusambaza maji kikamilifu katika maeneo ya shehia ya Kwamtumwajeni, Nyerere, Sogea, Magomeni na Meya.

(b) Kutokana na bomba hizo kutotoa maji kwa muda mrefu, kuharibika na nyengine kuziba kabisa na hata kupitiwa na baadhi ya miradi ya *BIG Z* katika shehia hizo, je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati njia hizo za maji ndani ya shehia hizo ili wananchi waweze kufikiwa na maji hayo katika nyumba zao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

491. MHESHIMIWA MOZA MOHAMED KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Vanila ilikuwa inauzwa kilo moja shilingi milioni moja, hali inayopelekea wakulima wengi kulima zao hilo. Hata hivyo, kwa sasa bei ya vanila imeshuka kwa sababu wafanyabiashara wasiowaaminifu kuichanganya vanila ya Zanzibar na ya Dar-es-salam katika Soko la Dunia ambayo imegundulika kuwa na sumu, huku ikifahamika juu ya ukweli kwamba vanila ya Zanzibar ni nzuri na iko salama.

Je, Serikali imejipanga vipi hatika kurejesha soko la vanila duniani ili kuondosha shaka ya kuwa ina sumu.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

306. MHESHIMIWA JUMA USONGE HAMAD (Jimbo la Chaani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ninaipongeza sana Serikali kwa kujenga skuli za ghorofa, kuziimarisha na kuwa za kisasa na zenye mazingira mazuri ya kusomea.

Je, ni lini skuli ya Pwani Mchangani Sekondari itafanyiwa marekebisho na kuwa nzuri na ya kisasa kama zilivyo skuli nyengine hapa nchini.

365. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali imechukua jitihada kubwa ya kuboresha miundombinu ya elimu ikiwa ni pamoja na kujenga majengo ya kisasa. Hata hivyo, kuna changamoto ya upungufu wa madarasa katika skuli ya Kiboje Mkwajuni.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza madarasa katika skuli ya Kiboje Mkwajuni.

**Wizara ya Afya:**

28. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kutokana na umuhimu mkubwa wa tiba asilia katika kuhifadhi na kuimarisha afya za wananchi, kupunguza utegemezi wa dawa za viwandani na gharama zake, pamoja na kuendana na rasilimali za asili zilizopo Zanzibar, kuna haja ya kuwepo kwa mfumo madhubuti wa kisheria, kitaasisi na kitaalamu wa kuimarisha matumizi ya tiba asilia kwa usalama na ufanisi.

(a) Je, Serikali imechukua hatua zipi mahasusi katika kuimarisha, kulinda na kutambua rasmi tiba asilia kama sehemu ya mfumo wa huduma za afya Zanzibar.

(b) Ni mkakati gani wa Serikali wa kuendesha na kuimarisha tafiti za kisayansi kuhusu ubora, usalama na ufanisi wa tiba asilia.

(c) Je, Serikali imepanga kuchukua hatua zipi katika kuunganisha tiba asilia na mfumo rasmi wa huduma za afya.

431. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni lini Serikali itaendelea kuajiri madereva wa kutosha katika Sekta ya Afya ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa madereva.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

37. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa eneo la Mji Mkongwe limekuwa na wakaazi wake ambao wanatumia vyombo vya usafiri na kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na ada ya maegesho mpaka katika maeneo wanayoishi watu na yale maegesho yaliyo mkabala na makaazi ya watu.

(a) Kwa nini kumekuwa na utaratibu wa kuweka ada za maegesho katika makaazi ya watu.

(b) Kwa nini yale maegesho yaliyo mkabala na makaazi ya watu na ambayo kabla ya kufanywa maegesho, wakaazi wa Mji Mkongwe wakiweka vyombo vyao, yasiondolewe ada kwa wakaazi hao.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda</u>:**

271. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Ni muda mrefu sasa, kiwanda kilichokuwa kinazalisha sabuni kilichopo Bopwe Wete Pemba kimekufa na kuwachwa gofu hadi kuta zake zimekuwa hatarishi kwa wananchi wa eneo hilo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukifanyia matengenezo kiwanda hicho ili kiweze kufanya kazi ipasavyo na kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

IV. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2026/2027.

**Waziri wa Afya:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**19 Mei, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**